BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 02 Machi, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed.
Hoja ya Mjumbe Kuhusu Ongezeko la Uingizaji na Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar.

Mheshimiwa Asha Abdalla Mussa
Hoja ya Mjumbe kuhusu kutoa Maazimio Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, Zanzibar.

II. MASWALI:

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

55. MHESHIMIWA ABDALLA MAULID DIWANI (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Pamoja na jitihada nzuri za kusambaza umeme katika sehemu mbali mbali za nchi kwa kuimarisha miundombunu ya umeme, lakini yametokea matukio ya

kuweka umeme huo hadi katika sehemu ambazo hazina mahitaji ya kawaida ya umeme.

a) Je, ni lini Shirika lako litaziondosha nguzo za umeme ambazo zimewekwa kwenye viwanja vya mpira vya Mnazi Mmoja.

b) Je, huoni kuwa tunaondosha haiba na malengo ya viwanja vile vya mpira kwa kuwekwa nguzo za umeme kwa muda mrefu.

66. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Uharibifu wa mazingira ni suala lililoathiri katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar hasa Wilaya za Magharibi na Kati. Uharibifu huo husababisha madhara makubwa kwa jamii na pia kuitia hasara Serikali kwa kuharibu miundombinu mbali mbali iliyowekwa.

Je, ni matukio mangapi ya uharibifu wa mazingira yaliyoripotiwa na hatua gani za kisheria zilizochukuliwa kwa wale waliothibitishwa kufanya makosa hayo.

<u>Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi :</u>

9. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Wakulima wa Wilaya ya Mkoani katika Bonde la Darajani lililoko Makombeni, kwa muda mrefu wanaidai Serikali kupitia Wizara ya Kilimo.

a) Je, ni kiasi gani wanachodai wakulima hao na ni wakulima wangapi wanasubiri malipo hayo mpaka sasa.

b) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kutolipwa kwa wakati wakulima hao wakati Wizara ina wataalamu wa Mipango ambao wanatakiwa kupanga na kuamua kabla ya utekelezaji wake kufanyika.

97. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba marehemu Salim Nassor Juma aliruhusu wananchi wanaotaka mashamba ya mikarafuu ya Serikali wafyeke na kupanda mikarafuu mipya. Lakini baada ya kufanya hivyo, wananchi hao sasa wameondoshwa kwa maelezo kuwa hawana nyaraka za mashamba hayo na kusababisha manung'uniko makubwa.

a) Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi mashamba hayo ili waweze kupanda mikarafuu zaidi.

b) Je, Serikali haioni kwamba kutowaachia wananchi kuyatumia mashamba hayo yaliyokuwa ya eka tatu hasa ya mikarafuu, kumepunguza ari ya kutimiza azma ya Serikali ya kuongeza kupanda mikarafuu.

c) Je, Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya mashamba tangu ilipoyarithi mashamba hayo kutoka Idara ya Ardhi, imeshapanda mikarafuu mingapi katika mashamba hayo wanayoyakodisha.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

43. MHESHIMIWA ABDALLA MAULID DIWANI (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika siku za karibuni kumekuwa na matumizi mabaya ya mitandao ikiwemo kusambazwa picha za ngono.

Je, hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu wanaofanya vitendo hivyo.

89. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia safi ya kuendeleza wananchi wake na miji yake katika maeneo takribani yote ya miji na yenye barabara, imeweka sheria

kwamba barabara kubwa (main road) ziwe na hifadhi ya barabara kwa mita 15 na barabara ndogondogo mita 8. Hata hivyo, barabara hizo kwa sasa zinaachwa na wananchi wanajenga bila kuzuiwa na wapimaji wa viwanja hivyo wamepima mpaka maeneo ya barabara.

a) Je, mpimaji eneo na mwananchi ni nani mwenye kosa.

b) Je, Serikali ni lini itaonesha mipaka ya barabara zake kwa vipimo ili wananchi wasiisogelee barabara na kuleta usumbufu wakati Serikali inapotaka kujenga barabara zake.

c) Je, Serikali haioni kuwa gharama za kupima barabara zake zote hivi sasa ni ndogo kuliko kusubiri mpaka wakati ambao Serikali itaamua kujenga barabara hizo na itakuwa zimeshajaa nyumba na kuzivunja ni gharama kubwa na kupelekea uhasama na wananchi.

III. HOJA ZA WAJUMBE:

Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed

Hoja ya Mjumbe kuhusu Ongezeko la Uingizaji na Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar.

Mheshimiwa Asha Abdalla Mussa

Hoja ya Mjumbe kuhusu kutoa Maazimio Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, Zanzibar.

Zanzibar,
02 Machi, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.